SIKU 30 ZA KUKUA

•KIROHO •KIAFYA •KIUCHUMI

TAFAKARI NENO,
TAMKA NENO,
POKEA HITAJI LAKO

UKUNDI E. MLELWA

SIKU 30 ZA KUKUA

KIROHO, KIAFYA NA KIUCHUMI

TAFAKARI NENO,
TAMKA NENO,
POKEA HITAJI LAKO

SIKU 30 ZA KUKUA

KIROHO, KIAFYA NA KIUCHUMI

UKUNDI E. MLELWA

MAFANIKIO
WORKSHOPS

SIKU 30 ZA KUKUA KIROHO, KIAFYA NA KIUCHUMI TAFAKARI NENO, TAMKA NENO, POKEA HITAJI LAKO

ISBN:978-9976-59-927-5

Hati miliki © 2019 Ukundi E. Mlelwa
P.o.Box 9690
Dar es Salaam

Haki zote za kunakili zimehifadhiwa

Jalada la mbele na nyuma na Ikechukwu Ejukwu

Kimeundwa na Trinity Idea Studios (T) Dar es Salaam

Kinasambazwa na Vowels Associates (T) Ltd Dar es Salaam,

KWA AJILI YAKO

KUTOKA KWA

YALIYOMO

Tabaruku	7
Utangulizi	8
Namna ya kutumia kitabu hiki	10
Kukua Kiroho	12
Kukua Kiafya	48
Kukua Kiuchumi	59
Tafakari	75
Maombi	76
Shuhuda	81
Kuhusu Mwandishi	87

TABARUKU

Kwa ajili ya wale wote wanaotamani kuishi maisha yanayo muakisi Yesu Kristo yenye ushindi katika nyanja zote za kiroho, kiafya na kiuchumi.

UTANGULIZI

Mara nyingi tunakuwa na mtazamo unaotufanya tushindwe kuwa huru katika kupata mafanikio ya kiroho, kiafya na kiuchumi. Na hii inatokana zaidi na dkra tulizonazo katika mawazo yetu.

Tukiwa ni watu wa kudkiri hasi tutapata mambo ya hasi ambayo ni woga wasiwasi na hata kushindwa na kuishiwa. Tunaweza kujifunza kubadili hali ya maisha yetu kwa njia ya kuanza kubadilisha dkra zetu kuwa chanya na kuwa na mtazamo chanya.

Kitabu hiki ni mahususi kwa kuwawezesha wale wanaotamani kuona mabadiliko makubwa ya kiroho, kiafya na kiuchumi kutokea katika maisha yao. Naomba ujue ya kuwa namna ulivyo sasa ni matokeo ya mambo uliyoweka kichwani mwako au mawazo yako kuhusu jambo fulani na kuliamini. Tukibadilisha mawazo na kudkiri tofauti na mazingira yetu, tutabadili hatma ya maisha yetu. Inawezekana kubadilisha hali ya maisha sasa, tukiamua kufanya hivyo.

Katika kitabu hiki tunakwenda kuona namna tunavyoweza kutumia neno la Mungu kwa njia ya kutamka kila siku na kuleta mabadiliko makubwa katika dkra zetu. Kwa kufanya hivyo, tutajikuta tunaanza kuamini zaidi ya kuwa tunaweza kukua kiroho, kiafya na kiuchumi, kwani neno la Mungu ni nyundo na ni upanga ukatao kuwili. Na ni hakika ya kuleta mabadiliko kwetu.

Anza kusoma kwa kutamka kila neno la siku hiyo, kila siku kwa kulitafakari na kuliamini na ndipo mabadiliko yataanza kutokea ndani yako na utaanza kuona ukianza kufanana na kile unachokitamka.

NAMNA YA KUTUMIA KITABU HIKI

Kila siku kuna sehemu tatu za kusoma na kutafakari. Unaweza kuamua kuanza kusoma kwenye kukua kiroho au kiafya au kiuchumi kutokana na hitaji lako. Kazi kubwa ni kutamka pale palipoandikwa Kiri na kupaweka kichwani ili kuweza kutamka popote na muda wowote tunapokuwa. Ni muhimu kuwa na maneno chanya na yenye kututia nguvu na imani katika midomo yetu kwani kwa kutamka na kukiri, ndipo ushindi huja.

Pale palipoandikwa Neno, ni mstari wa kusimamia huo ukiri ili malaika wa Mungu waweze kwenda kukuletea hicho unachokiomba au kutamka. Mungu anasema, analiangalia neno lake ili alitimize (Yeremia1:12). Na malaika wa Mungu husikiliza sauti ya neno la Mungu na kulitendea kazi (Zaburi 103:20)

Tunapokuwa tunafanya ukiri na kutamka mambo katika maisha yetu, watoto wetu, ndoa zetu, biashara zetu, kazi zetu, uchumi wetu na huduma zetu kutokana na neno la Mungu linavyosema, Mungu na Malaika nilazima walifanyie kazi ili kutupa hilo hitaji tunaloliomba au kutamka.

Nimuhimu sana tujue neno la Mungu kwa kichwa na kwenye moyo na kulitamka pale tunapolihitaji. Kwani kukiri au kutamka maneno ya Mungu ni kuipa imani yetu sauti. Na kwa kusema kwa sauti, milango ya fahamu itasikia na kuanza kuendana na kukubaliana na tunachokiamini. Jua ya kuwa Imani ni mlango wa hisia wa kiroho ambao ni mlango wa sita baada ya ile milango mitano ya fahamu. Tukizoea kufanya maamuzi kwa kupitia mlango huu wa kiroho, yaani Imani, tutakuwa sahihi mara zote na kufanikiwa kwa asilimia miamoja kuweza kukua kiroho, kiafya na kiuchumi pia.

TAMKA MANENO YA MUNGU ILI KUACHILIA MALAIKA KUKUPATIA HITAJI LAKO SASA!

KUKUA KIROHO



Kukua kiroho ni ile hali ya kuanza kufanana na Yesu Kristo. Ni hali ya kupenda mambo ya rohoni zaidi kuliko ya ulimwengu huu. Mambo ya rohoni yanatambulika zaidi katika matendo anayoyafanya au asiyoyafanya mtu. Ukianza kuwa mtu wa rohoni utaanza kupenda kufanya mambo yanayompendeza Mungu na kusikiliza sana sauti ya Roho Mtakatifu.

Pia utaanza kuona vile vitu ambavyo ulikuwa unavikimbilia sana vya dunia hii ni kama havina tena maana kwani umetambua ya kuwa Mungu baba na Yesu Kristo wanakutosheleza.

Ili kuweza kuwa mtu wa rohoni ni muhimu KUAMUA kuachana na tamaa za mwili, tamaa za dunia na pia kumpinga shetani katika kila analolileta kwetu.

Kwanamna hiyo tutaanza kuishi maisha ya ushindi na yenye kusudi ambalo ndilo Mungu alilotupangia hapa duniani.

2 Petro 1:3-8, inatuonyesha kuwa tukiwa ni watu wa rohoni, tunakuwa na uungu wa Mungu ambao unatukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa. Na ndani yake kuna ahadi kubwa mno na zenye thamani za kukusaidia katika maisha ya hapa duniani.

Hatua za kuweza kukua kiroho

Ili kuweza kubadilisha maisha yako kwa ujumla wake na kuwa mazuri na yenye staha na kupendeza, ni muhimu sana kuangalia hali yako ya kiroho. Ni muhimu sana uweze kukaa na kutafakari ya kuwa unataka kuishi kwa namna gani. Kuishi kidunia au ki Mungu.

Kama maamuzi yako ni kuweza kuishi kwa kumuakisi Mungu, basi pata nafasi ya kufuatisha hizi hatua nne muhimu katika kukuletea mabadiliko makubwa na mazuri katika maisha yako.

Kwanza, andika kwenye maazimio (resolutions) yako kuwa unataka kukua kiroho. Maazimio haya ni yale unayaweka kila baada ya muda fulani kuweza kutaka kutimiza malengo fulani ya kimkakati.

Pili, weka matamanio yako kuwa ya hali ya juu ya kutaka kuwa na ushirika mzuri na wa karibu na Roho Mtakataifu.

Tatu, tamani kumsikia Mungu akiongea nawewe kwa kupitia neno lake.

Nne, tamani kuishi maisha yanayompendeza na kumuakisi Mungu.

Ukiweza kuzifanyia kazi hizi hatua nne katika maisha yako, taratibu utaanza kuona mabadiliko makubwa yakimaisha yakianza kukutokea.

Utaanza kuona unapata uelewa wa hali ya juu wa neno la Mungu kila unapolisoma. Huu uelewa ni uvuvio wa neno au mwanga katika hilo neno na linakuwa linajibu maswali au swali lililokuwa linakutatiza kwa muda mrefu.

Utaanza kuona ukweli wa namna dhambi ilivyo mbaya na machukizo mbele za Mungu.

Utaanza kujua umuhimu wa kudkiri yaliyo mbele yako zaidi kuliko yale unayoyapitia hapa duniani.
Kwa kifupi unakuwa na nguvu ya kusoma neno, kuliishi na kuelezea wengine.
Kila utakachoomba kitakuwa kinajibiwa kwa haraka zaidi kuliko pale mwanzo.

SIKU YA 1

KUFANYWA UPYA NIA ZETU

Kiri: Fikra zangu na mawazo yangu yamegeuzwa na kuwa mapya. Ninajua mapenzi ya Mungu ni kunipa mema katika maisha yangu.

Neno: Warumi 12:2
"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kupendeza na ukamilifu."

Ili mawazo yetu na dkra zetu ziweze kufanywa upya kwa kutumia neno la Mungu, mambo yafuatayo yanatakiwa kufanywa:

1. Soma neno la Mungu kila siku
2. Tafakari hilo neno ulilolisoma
3. Omba kwa kutumia neno la Mungu kulingana na shida uliyonayo.

4. Usirudi nyuma kwenye mambo ya zamani ya kidunia.

5. Fikiri tu yaliyo ya juu ambako Mungu yuko.

Anza leo kubadili maisha yako kwa kutumia neno la Mungu.

SIKU YA 19

UKAMILIFU NA UNYOFU

Kiri: Ninakwenda njia ya ukamilifu na unyofu siku zote

Neno: Zaburi 25:21
"Ukamilifu na unyofu zinihifadhi..."

Tambua kuwa:-

1. Maisha ya ukamilifu hufungulia Baraka za Mungu alizoziahidi kwa ajili yako.

2. Kuishi maisha ya Ukamilifu maana yake ni kuwa mkweli, mwaminifu, ni kufanya mambo mazuri hatakama hakuna anayekuona.

3. Kuenenda kwa ukamilifu ni kuamua.

Anza leo kuishi maisha ya UKAMILIFU

SIKU YA 3

KUMTUMAINI BWANA

Kiri: Namtumaini Bwana katika kila eneo la maisha yangu.

Neno: Mithali 3:5
"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe;"

1. Amua kumtumaini Bwana katika kila eneo la maisha yako, wakati wa shida na wakati wa raha. Wakati wa kuweza na wakati wa kushindwa. Amini tu ya kuwa atakupa ushindi.

2. Amini ya kwamba Mungu anaweza kukutembelea katika shida yako na kuitatua kama vile alivyokuwa akiwatatulia shida wale watu wa kwenye biblia.

3. Kuwa na ujasiri wa kumwamini Yesu tu hata kama shida yako inaonekana mbaya kiasi gani,Yeye atafanya kutokana na kuamini kwako.

4. Ukimwamini Mungu na kumuachia afanye, utapata amani.

5. Mawazo yako yalenge kumtazama Bwana na siyo kutazama hali inayokuzunguka.

6. Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana (Yeremia 17:7)

SIKU YA 4

AMRI NA MAMLAKA

Kiri: Mimi ni kanisa la Mungu. Shetani hana nguvu juu yangu.

Neno: Luka 10:19
"Tazama nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui. Wala hakuna kitu kitakachowadhuru."

Tambua ya kuwa:-

1. Hauhitaji kuwa na hofu au woga juu ya shetani na nini anachokifanya juu yako, kwa watoto wako, na ndoa yako au kwenye kazi yako.Tunayo mamlaka ya kumshinda shetani.

2. Unahitaji kufanya mazoezi ya kutumia mamlaka uliyo nayo kila siku katika kumpinga shetani katika -

maisha yako.

3. Ukimkemea shetani kwa mamlaka uliyopewa na Bwana Yesu, atakimbia.

4. Mungu anatuona washindi katika Yesu Kristo. Nawe anza sasa kujiona mshindi katika kila eneo la maisha yako, na utakuwa hivyo.

SIKU YA 5

KUWA KICHWA, KUWA JUU

Kiri: Mimi ni kichwa, Mimi niko juu.

Neno: Kumbukumbu la torati 28:13
"Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini."

Tambua ya kuwa:-

1. Wewe kuwa kichwa na kuwa juu kunategemea na namna unavyolishika neno la Mungu. Kumbukumbu la torati 28:1

2. Ukiona mambo yako hayaendi kama unavyoomba, huenda kuna mahali hujakaa sawa na Mungu. Mungu si mwanadamu aseme uongo.Wewe ndiyo utakuwa haujakaa sawa.

3. Ukisha gundua mahali ulipoacha mlango wazi katika maisha yako na shetani akaingia, omba toba na ufunge huo mlango.

4. Anza kutamka kwa mamlaka ya kuwa wewe ni kichwa tu na uko juu tu, na utakuwa hivyo

SIKU YA 6

ROHO YA UPENDO NA NGUVU

Kiri: Nina roho ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa kiasi

Neno: 1Timotheo 1:7
"Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi."

Tambua ya kuwa:-

1. Woga na wasiwasi ndiyo chanzo kikubwa cha wakristo wengi kushindwa kuishi maisha ya ushindi.

2. Ukiendelea kuwa na hofu yakuwa mambo mabaya yanaweza kukujia, yatakujia hakika.

3. Woga huwafanya wakristo kushindwa kutembea katika nguvu na mamlaka ya Mungu

4. Woga huleta laana kutoka kwa adui, na Imani huleta Baraka kutoka kwa Mungu

5. Ili kutembea mbali na hofu, unatakiwa kuacha kuangalia vitu vinavyoonekana na kuangalia vile visivyoonekana kwa kutumia Imani. (2 Wakorintho 4:18)

SIKU YA 28

NAYAWEZA YOTE KATIKA YESU KRISTO

Kiri: Nayaweza mambo yote katika Yesu anitiaye nguvu.

Neno: Wadlipi 4:13
"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."

Kama mtu uliyempokea Yesu, unao uwezo wa kufanya chochote unachokitamani au unacho kitarajia kwa kwakuwa unao upako na nguvu ya Kristo ndani mwako.

Unachohitaji kufanya ni kuamini ya kuwa yote unayoyatamani ambayo ni mapenzi ya Mungu yanakwenda kutendeka katika maisha yako.

Ni mapenzi ya Mungu wewe uwe na afya njema, uwe na familia nzuri, uwe na ndoa nzuri, uwe na kazi nzuri, uwe na fedha za kutosha , uwe mkweli, uwe mtakatifu, uwe na hekima, uwe na kibali, uwe tajiri, uwe na upendo, uwe mkamilifu nk.

SIKU YA 8

KIMBILIO NI YESU

Kiri: Nimefunikwa na mbawa za Bwana. Ninalo kimbilio.

Neno: Zaburi 91: 4
"Kwa manyoya yake atakufunika, chini ya mbawa zake utapata kimbilio"

Hakuna kitu kizuri kama kuwa na uhakika wa usalama hapa duniani.Tunaona hali ya kiuchumi na kidkra na kimahusiano inavyozidi kushuka siku hadi siku.Watu wengi wanapata shida na woga na wasiwasi wa nini kinaenda kutokea hapo baadae. Lakini wewe mtu wa Mungu, uliye na Yesu Kristo ndani ya maisha yako, hauhitaji kuwa mtu wa hofu au mashaka au wasiwasi. Unalo kimbilio. Kimbilio lako ni Yesu.

Ameahidi kutupa uvuli wake yeye mwenyewe. Unapaswa kumuamini na kumuachia yeye maisha yako, huku ukiondoa hofu kwa maana hofu zote hutoka kwa shetani. Mungu wetu anakaa mahali penye amani kwahiyo ili uweze kumlingana Bwana unatakiwa uwe ni mtu wa amani siku zote.

Kumbuka Imani ukiondoa hofu utapata Amani.

Achana na hofu leo!

SIKU YA 3

WEMA NA FADHILI

Kiri: Wema na fadhili zinanifuata sasa katika maisha yangu.

Neno: Zaburi 23:6
"Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu"

Ni muhimu kujua ya kuwa chochote kinachotokea katika maisha yako, haijalishi ni kizuri au kibaya, Mungu ni mwema. Fahamu ya kuwa Mungu hapendi wewe upate shida, kwani shida nyingi zinatoka kwa shetani.

Mungu ametupa nguvu ya kumpinga shetani, ni kazi yako kutumia nguvu hiyo na mamlaka kwa jina la Yesu na kumpinga shetani katika mazingira yanayokuzunguka.

Amini ya kuwa wema wa Bwana unakuzunguka.
Usiogope!

SIKU YA 10

MUNGU HUJISHUGHULISHA NAMI

Kiri: Ninamtwika Yesu fadhaa zangu zote sasa

Neno: 1 Petro 5:7
"Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu."

Mahangaiko ya ulimwengu huu unawafanya wanadamu wasipate muda wa kulitafakari neno la Mungu.

Ukiwa umejawa na neno la Mungu moyoni mwako, inakuwa rahisi kuwa na imani ya kumuachia Mungu kila kitu kwenye maisha yako. Usipokuwa na muda wa kulitafakari neno la Mungu, mahangaiko ya dunia hii yatakuchota na kukukandamiza chini.

Mahangaiko ya dunia hii yanakufanya usizae matunda ya kimungu maishani mwako.

Ni wewe unayetakiwa kuamua kukabidhi yote kwa Yesu huku ukiendelea kuimarika katika neno lake.

Kiri ya kuwa hutashiriki katika hofu inayotokana na taarifa mbaya iliyomo duniani kama habari mbaya za magonjwa, kukosa kazi, elimu kushuka, majanga mbalimbali, huzuni mbalimbali nk.

SIKU YA 34

UPENDO WA MUNGU

Kiri: Nina upendo wa Mungu ndani yangu.

Neno: Wimbo Ulio Bora 2:4
"Na bendera yake juu yangu ni Mapenzi"

Upendo ni silaha ambayo shetani hawezi kuishinda. Upendo wa Mungu ndani yako hukufanya uwapende watu wengine bila kikomo.

Kwakuwa na bendera ya Mapenzi ya Mungu juu yako, ina maana tunatakiwa kuishi kwa kiwango hicho cha upendo wa Mungu na si kwa kiwango cha matakwa yetu.

SIKU YA 12

UFALME WA MUNGU

Kiri: Ninatafuta kwanza Ufalme wa Mungu katika maisha yangu.

Neno: Mathayo 6:33
"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa"

Kama tukitafuta ufalme wa Mungu kwanza katika maisha yetu, Mungu anakwenda kushughulika na mambo yetu. Naye atafungua milango ya kupata zaidi kutoka kwake.

Kutafuta ufalme wa Mungu na mapenzi yake, ni kujiongeza katika kumjua Mungu.

Unatafuta Ufalme wa Mungu kwa kulisoma neno lake na kulifuata linavyosema. Ndipo utaanza kukua katika maeneo yote ya kiuchumi, kiafya, kielmu na kuwa huru katika maisha yako kwa ujumla.

Ufalme wa Mungu unafanya kazi kwa mfumo wa kupanda na kuvuna. Ukipanda mbegu ni lazima utavuna kitu. Ukipanda upendo utavuna upendo, Ukipanda pesa utavuna pesa, Ukipanda uradki utavuna maradki. nk.

SIKU YA 37

KUTHIBITIKA KATIKA HAKI

Kiri: Nimethibitika katika haki. Sitaonewa na chochote..

Neno: Isaya 54: 14
"Utathibitika katika haki; utakuwa mbali na kuonewa, kwa maana hutaogopa na mbali na hofu, maana haitakukaribia."

Mungu amesema utathibitika katika haki, na utakuwa mbali na kuonewa. Katika maisha yako ni muhimu kujua haya. Unatakiwa kutamka hivi kila unapopata shida au matatizo yanayokuzunguka. Haijalishi ni jambo gani liko mbele yako. Simama na neno la Mungu na ndipo utapata ushindi.

Ondoa hofu kwa maana hii ndiyo silaha ambayo shetani anaitumia kuweza kukupata. Usipokuwa na hofu, mabaya huondoka yenyewe.

SIKU YA 14

MAJINA YAMEANDIKWA MBINGUNI

Kiri: Ninaishi maisha ya wokovu. Jina langu limeandikwa mbinguni

Nemo: Luka 10:20
"Lakini msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwasababu majina yenu yameandikwa mbinguni."

Wewe unayefanya kazi ya Mungu, iwe ni kuhubiri, kuimba, kuomba, kufunguwa watu vifungo mbalimbali nk.Tunakumbushwa ya kuwa tunatakiwa kujinyenyekeza zaidi na tusione kuwa tumefanikiwa sana. Kumbe mafanikio makubwa tunayotakiwa kuwa nayo ni majina yetu kuandikwa mbinguni.

Tujiulize kila siku na kila saa je jina langu limeandikwa mbinguni? Kwa namna hii tutakuwa ni watu wa kuishi maisha ya kiroho zaidi kuliko ya kimwili.

Kiri neno hili kila siku na utaona polepole ukibadilika na kuwa mtu wa rohoni inayokusaidia kujiandaa na ulimwengu ujao mbinguni.

SIKU YA 40

UZIMA WA MILELE

Kiri: Mimi namwamini Yesu Kristo, ninao uzima wa milele.

Neno: Yohana 3:16
"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwana wake wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele."

Watu wengi tunatamani kuiona mbingu au kumuona Mungu hapo siku zijazo. Lakini tunasahau kuwa kuna njia moja tu ya kuweza kuipita ili kumwona Mungu. Njia ni Yesu Kristo. Ukimwamini Yesu unapewa uwezo wa kufanyika mwana wa Mungu na hivyo kupewa mastahili yote yatakayokuwezesha kuishi maisha yanayopelekea wewe kumuona Mungu.

Mwamini Yesu leo uweze kuingia kwenye mlango mwembamba uelekeao uzimani.

SIKU YA 16

KUHUBIRI INJILI

Kiri: Ninaleta watu kwa Yesu

Neno: Marko 16:15
"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe."

Kazi kubwa ambayo tumeachiwa kuifanya kama wakristo ni kuihubiri injili ya Yesu Kristo kwa kila mtu. Ili atakae amini asipotee. Tunatakiwa kumuishi Kristo na kueleza watu habari za Yesu kila tunapokuwa. Je watu wanakujua ya kuwa umeokoka? Je wanamwona Yesu katika maisha yako?

Ni muhimu kuwa barua njema kwa wanaotunzunguka kwani unaweza kumbadilisha mtu kwa upendo ulionao, kwa amani uliyo nayo, kwa utu wema na fadhili uliyo nayo. Ni muhimu pia kueleza watu wanaokuzunguka ubaya wa dhambi na namna itakavyowatenga na Mungu.

Anza leo kueneza injili ya Bwana ili atakapokuja uweze kutoa hesabu nzuri mbele zake.

SIKU YA 43

ULIMWENGU WA ROHO

Kiri: Nina keti na Kristo katika ulimwengu wa roho.

Neno: Waefeso 2:6
"Akatufufua pamoja nae, akatuketisha pamoja nae katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu."

Mtu aliyempokea Kristo amefanyika sawa na Kristo. Sisi si watumwa wake bali sisi ni ndugu zake. Alipo Yesu nasi ndipo tulipo kiroho. Basi imetupasa kuishi kwa ujasiri na kwa kutumia mamlaka ya kiungu tuliyonayo ili kuweza kusambaratisha hila zote za yule mwovu.

SIKU YA 18

KUSAMEHE NA KUSAMEHEWA

Kiri: Mimi nimesamehe wote na yote. Nimesamehewa pia.

Neno: Mathayo 6:14-15
"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipo wasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu."

Tunatakiwa tujitahidi sana kusamehe wengine na pia kujisamehe wenyewe. Kwa maana kwa kutokusamehe tunajiharibia wenyewe zaidi.

Tuangalie mfano wa Stephano ambaye aliweza kuwa na nguvu ya kusema Baba wasamehe makosa haya na wala usiwahesabie hatia.

Ili uweze kudkia kama Stephano alivyoweza kumudu kusamehe, nilazima uwe na uhusiano mzuri na Yesu Kristo. Bwana Yesu ndiye chanzo cha msamaha. Alikusamehe wewe bure ukiwa katika dhambi na sasa anataka na wewe usamehe wengine bure. Hii nguvu ya kusamehe inatoka kwa uwezo wa Roho mtakatifu pekee.

Unahitaji kuwa na ushirika mzuri na Roho Mtakatifu ili aweze kukusaidia kuondoa uchungu ulioko moyoni unaokusababisha kushindwa kusamehe. Amua kuwa na hamu ya kusamehe na umuombe Mungu akupe nguvu ya kusamehe kama ya Yesu na Stephano.

Tafakari neno la Mungu kuhusu kusamehe, na mara utaona furaha na upendo wa kimungu ikikujia. Utaanza kuwaonea huruma na kuwapenda wale uliokuwa unawachukia.

SIKU YA 19

UTAKATIFU

Kiri: Mimi ni mtakatifu kama Baba wa mbinguni alivyo mtakatifu

Neno: 1 Petro 1:15
"Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote;"

Utakatifu ni muhimu sana katika maisha yetu kwani ndicho kigezo cha kumuona Mungu.Tunatamani sana kumuona Mungu lakini mara nyingi hatudkirii ni kwa namna gani tunatakiwa kuishi ili tuweze kumuona Mungu. Kuna hatua muhimu sana ambayo itakusaidia wewe unayetamani kuishi maisha ya utakatifu hapa duniani. Kwani utakatifu duniani unawezekana na Mungu mwenyewe anasema anapendezwa na watakatifu waliopo duniani (Zaburi 16:3).t

1. Mpokee Kristo ndani ya maisha yako.
2. Jazwa na Roho Mtakatifu.
3. Anza kusoma neno la Mungu na kulitafakari
4. Tafakari mwisho wako unaoutaka uupate, yaani kumuona Mungu mbinguni.
5. Anza kutafuta mistari ya biblia inayokufundisha nini cha kufanya au nini si cha kufanya ili kuurithi uzima wa milele.
6. Anza kufanyia kazi ulichokisoma kwenye biblia
7. Tafakari uzuri wa kule mbinguni na tamani kupaona siku moja.
8. Tafakari ubaya wa jehanamu na namna usivyotaka kuenda huko.

Kwa kufanya hivi utaanza kuachana na vile vitu vyote vitakavyokufanya ukose mbingu. Hamu yote ya dhambi itaondoka na utaanza kuishi maisha yanayompendeza Mungu.

KUKUA KIAFYA

Kwa habari ya afya yako ni muhimu kujua yakuwa,

• Ni mapenzi ya Mungu wewe kuwa mzima na mwenye afya. (Isaya 53:4-5)

• Magonjwa yote yanatoka kwa shetani (Matendo 10:38)

• Mungu amedhihirisha uponyaji katika agano la kale na pia katika agano jipya

• Unaweza kupona sasa ukiamini neno la Kristo.

• Tafuta ukweli katika neno la Mungu, Amini ukweli huo juu ya uponyaji wako, Pokea uponyaji wako kwa imani.

Hatua za kuweza kukua kiafya

Ili kuweza kukua kiafya unatakiwa kufanya mambo yafuatayo.

Kwanza, Tafuta maneno ya kwenye biblia yahusuo uzima na uponyaji.

Pili, kiri kwa sauti mistari hiyo inayohusu uzima na uponyaji kutoka kwenye biblia

Tatu, Anza kutafakari juu ya uponyaji wako na uzima wako kwa kupitia damu ya Yesu Kristo iliyomwagika pale msalabani kwa ajili yako.

Nne, Pokea uzima na uponyaji uliofanyika kwako toka Yesu alipomwaga damu yake pale msalabani.

Tano, amini tu ya kuwa wewe ni mzima wa afya.

Sita, Kama kuna ripoti yoyote ambayo umepewa kinyume na neno la Mungu kuhusu afya yako, ichukue na uende mbele za Mungu kwa maombi ya kumshukuru kwa uponyaji au uzima wako. Halafu ikatae kwa nguvu zako zote ripoti hiyo mbaya. Fanya kwa kumaanisha.

Saba, ondoa woga na hofu. Hofu inatoka kwa shetani ili aweze kukupata kirahisi. Kataa hofu yoyote maishani mwako na kiri ushindi tu kwa kutumia neno la Mungu.

Nane, tafuta mtu wa Imani muweze kuomba pamoja. Nimuhimu kuwa na mtu wa karibu anayeomba kwa ajili yako.

Tisa, Kuwa na mazoea ya kumsifu na kumuabudu Mungu mara kwa mara. Mungu hukaa katikati ya sifa. Utahudumiwa kwa wepesi.

SIKU YA 53

KUWA NA AFYA

Kiri: Nina Afya na uzima maishani mwangu

Neno: Jeremia 30:17
"Maana nitakurudishia afya, Nami nitakuponya jeraha zako, Asema Bwana..."

Kwa wewe mtu wa Mungu uliyepatwa na ugonjwa unaokusumbua, amini ya kuwa Yesu pale msalabani alikusamehe maovu yako yote, na alikuponya magonjwa yako yote (Zaburi 105:3). Kazi yako ni kuamini ya kuwa kama vile alivyokusamehe, amekuponya pia.

Usiangalie ripoti ya daktari inasema nini. Macho yako yatazame Yesu anasema nini na ulipokee neno la Mungu katika moyo wako na akili zako na anza kujiona umepona. Anza kuchukua hatua za kiimani kwa kuanza kuona ukifanya yale mambo ambayo utafanya kama uko mzima. Fikiri hayo tu na uondoe hofu. Hakika kwa kufanya hivyo utapona.

SIKU YA 54

BARAKA KATIKA CHAKULA

Kiri: Ninamtumikia Mungu, Nitakuwa mzima siku zote.

Neno: Kutoka 23:25
"Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu, naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; Nami nitakuondolea ugonjwa kati yako."

Unajua uzima na laana vyote vinapatikana katika kukiri. Ukiwa unakiri uzima utapata uzima. Ukiwa unakiri laana, utapata laana. Kuwa makini sana na nini unachokitoa katika midomo yako kwani ndiyo hatima yako itakavyokuwa. Jifunze kukiri mema nayo mema yatakujia, haijalishi mazingira yako yakoje. Mungu ameahidi ukimtumikia atakuondolea ugonjwa. Pokea neno hili leo unapolitafakari na kulitamka.

SIKU YA 55

MABAYA HAYATAKUPATA

Kiri: Mabaya hayatanipata mimi, wala magonjwa hayata ikaribia nyumba yangu.

Neno: Zaburi 91:10
"Mabaya hayatakupata wewe; Wala tauni haitaikaribia hema yako"

Kila siku ya maisha yako ni muhimu kuomba au kukiri hivi. Duniani kuna mambo mengi ambayo yanatokea yenye kutuumiza kama magonjwa (tauni) na adha mbalimbali. Maadui pia ni wengi wasiopenda kukuona ukifanikiwa nk. Unapokiri mabaya hayatakupata ni kama unatengeneza wigo ambao utakulinda na mabaya yasi-weze kukuingilia maishani mwako. Ukizoea kutamka namna hii, utaanza kuona ukiwa huru na matatizo mengi yataisha.

SIKU YA 23

TULISHAPONYWA

Kiri: Nimeponywa kuanzia utosini mwangu mpaka katika viganja vyangu vya miguu.

Neno: 1 Petro 2: 24
"Na kwa kupigwa kwake, mliponywa"

Wewe uliyempokea Bwana Yesu katika maisha yako, uponyaji ni wa kwako. Kwani siyo tu Yesu Kristo alitupatia uponyaji wa rohoni yaani kuondolewa dhambi, bali pia alitupatia uponyaji wa mwilini.

Ukiri wa uponyaji kila siku ni muhimu kwa kuweza kukuletea matokeo mazuri katika mwili wako. Kwa jinsi unavyokiri uponyaji kwa kutumia neno la Mungu ndipo imani yako kwake hukua na kuleta kile unachokitaka.

Unapokuja kwa Yesu tegemea kupata wokovu katika nyanja zote za maisha.

Imani unayotumia kupata wokovu ni hiyo hiyo utakayotumia kuponywa magonjwa. Amini leo umeponywa.

SIKU YA 24

UJANA UNAREJESHWA

Kiri: Mimi nina nguvu, nina afya nina uzima

Neno: Zaburi 103: 5
"Aushibisha mema uzee wako. Ujana wako ukarejeshwa kama tai;"

Mara nyingi tunaona mtu mzee ni mtu aliyechoka, aliyekata tamaa na maisha na mwenye taabu nyingi. Mungu anasema ataushibisha uzee wako. Kama unamtegemea Mungu hata uzee wako utakuwa heri, utakuwa na manufaa, utakuwa na mchango kwa jamii na kuweza kuishi maisha ya matumaini. Uzee ni tunu kama ukiwa umeshajifunza mambo ya Mungu wakati wa ujana, kwani utakufanya uishi kwa heshima na kwa neema ya Mungu.

Unaweza kuwa mzee na kuwa na nguvu kama kijana. Kiri neno hili la urejesho uanze kuimarika katika afya yako ya mwili sasa.

KUKUA KIUCHUMI

Biashara na Fedha

Makazi na Usadri

Utalii

Watu wa Mungu, ni muhimu kujua kusudi la Mungu kwetu. Mungu anacho kitu ameweka ndani yetu ili tuweze kuleta matunda kwa ajli ya utukufu wake. Ili kuweza kufanikisha kusudi la Mungu maishani mwetu ni lazima kuifanyia kazi ile kusudi aliloliweka ndani ya kila mmoja wetu.

Tunatakiwa kufanya kazi (self production) inayopelekea kuonyesha ujuzi uliyowekewa ndani yako na Mungu.Tukiangalia zile ahadi 4 ambazo Mungu alimpa Adam na Hawa kwenye (Mwanzo 1:28). Nazo zinasema hivi. Zaeni (be fruitful), mkaongezeke (multiply), mkamiliki (replinish) na mkatawale (subdue).

Kumbe Mungu alishatupa uwezo ndani yetu wa kupata, kuongezeka, kumiliki na kutawala. Je ni kitu gani unafanya kinachofanya upate, uongezeke, umiliki na utawale?
Ni kazi ya kila mmoja wetu kutafuta nini Mungu ameweka ndani yake ili akue kiuchumi

Hatua za kuweza kukua kiuchumi

Kwanza, jifunze neno la Mungu linalohusu kufanikiwa. Katika biblia kuna manabii wengi ambao wameandika kuhusu kufanikiwa kwetu katika maisha haya ya hapa duniani. Anza kuchukua neno moja baada ya lingine linalohusu kupata fedha na mali na uyatafakari. Ukianza kujiona kuwa uko hivyo kama neno linavyosema, hatimaye utakuwa hivyo.

Neno la Mungu linasema utakuwa kichwa na siyo mkia. Utakopesha mataifa na hutamkopa mtu. Tukiangalia haya ni maisha ya mtu aliyefanikiwa kiuchumi na ndivyo ninaamini unatakiwa kuwa.

SIKU YA 25

KUBARIKIWA NA KUZIDISHWA

Kiri: Mungu ananibariki na kunizidisha sasa

Neno: 1Mambo ya Nyakati 4:10
"Huyo Yabesi akamlingana Mungu wa Israel, akisema, Lau kwamba ungenibarikia kweli kweli na kunizidishia hozi yangu…"

Tunamuona Yabesi akimuomba Mungu ambariki kimiujiza. Na Mungu mwenyewe alimuongeza katika kila nyanja ya maisha yake.

Ukimuomba Mungu, anaweza kukupa zaidi ya vile ambavyo unawaza. Yabesi anamtegemea Mungu katika utajiri wake na kuongezeka kwake katika maswala yake ya kiuchumi na fedha. Yabesi anajua ya kuwa Mungu ndiyo chanzo kikuu cha utajiri kwa maana baraka yake hukupa utajiri.

Je, unategemea nini katika kukupa uchumi mzuri ? Je ni dunia hii, watu au shetani? Anza leo kwa kumaanisha kumtegemea Mungu akubariki na kukuzidishia kwa kuomba sala hii ya Yabesi uweze kuleta mabadiliko katika maisha yako.

SIKU YA 26

HAZINA ZA GIZANI

Kiri: Hazina za gizani na Mali za sirini zinanifuata sasa.

Neno: Isaya 45:3
"Nami nitakupa hazina za gizani, na mali zilizofichwa za mahali pa siri…"

Kama mwana wa Mungu, Umeahidiwa na Mungu kupata vilivyo vyema. Unachotakiwa kufanya ni wewe kuwa na matamanio ya hivyo vitu vyema ambavyo unadkiri unataka vikutokee au uvipate katika maisha yako. Anza kuamini yakuwa Mungu atakupa. Ni hakika atakupatia.

Hazina za gizani na mali zilizodchwa zinaweza kuwa ni vile vitu unavyovitamani vikutokee katika maisha yako ambavyo bado havijatokea. Je unatamani maisha ya namna gani? Ukitumia neno hili kama njia ya kumkumbusha Mungu, atakupa.

Kumbuka hazina na mali zimetuzunguka. Mungu hazidchi ili tusizione. Bali amezidcha kwa ajili ya kuja kukupa wewe utakaye mwomba.

SIKU YA 27

KUZAA MATUNDA

Kiri: Ninafanikiwa katika kila jambo nilitendalo.

Neno: Zaburi 1:3
"Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji. Uzaao matunda yake kwa majira yake. Wala jani lake halinyauki. Na kila alitendalo litafanikiwa."

Tukiangalia neno mojamoja tunaona yakuwa huu mti umepandwa na siyo kuwa umejiotea wenyewe. Mti uliopandwa unaweza kuwa umepata matayarisho ya kutosha ambayo ni udongo mzuri wa kupandia, mbolea na kupandwa katika majira yake. Hii inatufundisha hata katika maswala ya roho zetu tunatakiwa tuwe na matayarisho mazuri ya mapema ya kuweza kupanda mbegu njema ambayo ni neno la Mungu katika maisha yetu. Tusisubiri mpaka tumesha pigwa na kutoswa na dunia ndiyo tuanze kutafuta neno la Mungu.

Kwanjia ya kusoma neno la Mungu na kuliishi, kutatufanya kuzaa matunda ambayo ni kufanikiwa maishani na hatimaye utukufu unamrudia yeye Yesu.

Anza kuona ukizaa matunda kwa majira yake. Anza kuona ukifanikiwa katika kila unalolitenda.

SIKU YA 28

BARAKA YA BWANA

Kiri: Nina baraka ya Bwana maishani mwangu

Neno: Mithali 10:22
"Baraka ya Bwana hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo."

Mtu aliyebarikiwa na Bwana ni mtu yule anayejua ya kuwa Mungu ndiye pekee wa kutegemewa ili kupata utajiri. Huyu mtu hategemei kazi, maradki, mzazi, mjomba, elimu ili kufanikiwa. Ukishajua chanzo chako cha mafanikio ni Mungu, basi utaanza kuutafuta ufalme wa Mungu kwanza.

Ufalme wa Mungu unatafutwa kwa namna gani? Ufalme wa Mungu unatafutwa kwa kufanya mapenzi ya Mungu yale yanayomgusa Mungu kukubariki. Malaki 3:10 inasema toa fungu la 10 na sadaka na madirisha ya mbinguni yatafunuliwa kwako.

Kumbukumbuka la torati 28:8 inasema “Bwana ataiamuru Baraka ikujie…” na si wewe uifuatilie Baraka. Kwa kufanya mapenzi ya Mungu unafungulia Baraka ya Mungu maishani mwako ambayo haina huzuni.Watu wengi ni matajiri na wamebarikiwa lakini wana huzuni. Huwenda baraka wali-zonazo wamezitafuta wenyewe na si kwa kumtegemea Mungu.

SIKU YA 29

KUPATA FAIDA

Kiri: Ninapata faida katika kila ninachofanya.

Neno: Isaya 48:17
"Bwana mkombozi wako, mtakatifu wa Israel asema hivi, Mimi ni Bwana, Mungu wako, nikufundishae ili kupata faida…."

Mungu wetu anapenda tupate faida katika maisha yetu na ndiyo maana katika kila mifano aliyokuwa akitoa ni ya kufanya biashara na kuleta faida. Na yule aliyeshindwa kuleta faida alinyanganywa na kuadhibiwa.

Je maisha yako yamejaa faida au hasara? Kile ulichokuwa nacho mwaka juzi kimeongezeka au kimepungua? Ni muhimu kutafakari maneno ya Mungu kwani ni kioo cha kutufanya kujiona tuko wapi na kama tunaenenda kama anavyotuagiza.

Kama unaona hupati faida katika unachokifanya basi tafakari hili neno na ulikiri kila siku ili liweze kukuletea imani na kuanza kukuletea mabadiliko katika maisha yako. Inawezekana kupata faida!

SIKU YA 30

UTAJIRI NA MALI

Kiri: Nina utajiri na mali nyumbani mwangu.

Neno: Zaburi 112:3
"Nyumbani mwake mna utajiri na mali."

Neno la Mungu linasema Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.

Je unaona nini nyumbani mwako?

Unaona utele au upungufu? Mara nyingi mtu huona zaidi asichonacho. Sasa anza kubadili mtazamo wako na dkra zako. Anza kuona mema yakikujia. Anza kuona vile vitu unavyovitamani viwepo nyumbani kwako. Anza kuona watoto wenye heshima na adabu, magari unayoyapenda, fedha, mashamba, nyumba, biashara. Anza kuona maisha unayoyatamani yakikujia na uanze kuyafurahia sasa.

Utaupata utajiri kwa njia ya kufanya kazi (self production), kutamani (desire), kukiri, kutegemea kuvipata na huku ukivifurahia kana kwamba umeshavipata (Marko 11:24)

Tafakari katika kukua kiroho/kiafya/kiuchumi

Je unayo matamanio (desire) ya kuishi maisha ya namna gani?

Anza kuyaandika chini katika karatasi na kuyasoma kila siku.

Tengeneza picha (vision board) ya vitu vyote unavyotaka vitokee katika kipindi hiki.

Andika vitu 300 ambavyo unatamani vitokee katika maisha yako. (hutakosa asilimia 10)

Anza kutafakari utakavyokuwa unafanya kusudi lakosasa.

Anza kuona ukiwasaidia watu katika shida zao.

MAOMBI

Sala ya Toba

Bwana Yesu, nakuja mbele zako kwa moyo wangu wote na kwa akili zangu zote. Ninaamini ulikufa msalabani kwa ajili yangu. Nakupokea sasa ndani ya moyo wangu na maishani mwangu. Naomba unisamehe dhambi zangu zote. Damu yako ya thamani inioshe na kunitakasa, iniweke huru sasa mbali na dhambi. Niponye na magonjwa yote. Nijaze na Roho Mtakatifu. Ondoa jina langu katika kitabu cha hukumu, andika jina langu katika kitabu cha uzima. Ninaamini na kupokea haya niliyoomba katika jina la Yesu Kristo, Amen

Maombi Ya kukua kiroho

Baba wa mbinguni, umetuita ili tuweze kuingia kwenye neema yako ya ajabu, ili kukua katika kumjua Yesu Kristo. Bwana Yesu haya ndiyo matamanio yangu yaani kukujua wewe zaidi na kuishi maisha yanayokupendeza wewe na yenye kumzalia Mungu matunda.
Roho Mtakatifu uonaye sirini na unayejua mapenzi ya Mungu, nisaidie kuondoa kila kisichofaa machoni pa Mungu na unifanye kujua nini cha kufanya au si chakufanya katika maisha yangu.
Kuanzia leo nitajifunza kumsikiliza Roho Mtakatifu nakufuata maagizo yake hatakama yatakuwa ni kinyume na kile nilichokizoea. Katika jina la Yesu Kristo. Amen.

Maombi Ya kukua kiafya

Katika jina la Yesu, na katika nguvu na uweza wa Mungu baba, ninaamuru magonjwa yote yaliyomo katika mwili wangu kuondoka sasa na kuenda katika miguu ya Yesu Kristo. Eenyi magonjwa, kazi zenu ndani ya mwili wangu imekwisha sasa. Ninaamuru maumivu ya kila aina kuondoka katika mwili wangu sasa. Ninaamuru roho zote za kansa, udhaifu, vidonda vya tumbo, uvimbe, uchovu, ukimwi, ugonjwa wa mgongo, kisukari, Ugonjwa wa moyo, magonjwa ya akili, kusahau, shida ya mapafu, shida ya neva, shida ya ubongo kuachilia mwili wangu sasa katika jina la Yesu.

Asante Bwana Yesu kwa nguvu ya uponyaji. Naomba uwatume malaika wako wakunihudumia ili waweze kuniondolea chochote kwenye mwili wangu kilichotokana na dhambi, magonjwa na hila zote za adui shetani. Tuma roho wako mtakatifu anijaze na furaha, mwanga na Amani. Amen

Maombi Ya kukua kiuchumi

Baba wa mbinguni, nashukuru kwa ahadi zako za kutufanikisha sisi na uzao wetu. Mungu umesema yakuwa utatupa zaidi ya kile tunachokiomba kama tukitoa fungu la 10 na kufuata njia zako.

Kutokana na neno lako la Malaki 3:10 umeahidi kunifungulia madirisha ya mbinguni na kunimwagia baraka. Nami ninatoa fungu lako la 10 na kufuata njia zako. Kwa kupitia jina la Yesu Kristo, ninaomba baraka yako ya kifedha inijilie sasa ya Tzs_____

Ninaamini na kuzipokea sasa katika roho yangu na hakika zimekuwa halisi kwangu.

Nakurudishia sifa heshima na adhama kwa kuwa umetenda. Amen

SHUHUDA

Ushuhuda wa Kwanza

Ninaandika kushuhudia namna madarasa yako ya ushauri yalivyonisaidia.

i) Sikuwa na ndoa nzuri, kwa kupitia ushauri wako niliweza kuelewana na mke wangu na sasa tunaishi maisha mazuri na yenye upendo.

ii) Nilikuwa na matatizo ya kiuchumi kutokana na kupata hasara kazini iliyopelekea ushukaji ari wa kazi na hatimaye kuacha kazi. Kutokana na ushauri wako wa namna ya kudhibiti msongo wa mawazo, nilipata amani na mpenyo wa kuweza kushinda mambo yote yaliyokuwa yananikabili kazini.

iii) Kwa kupitia goal setting training uliyofundisha, niliweza kuanza kupanga kazi zangu vizuri hatimaye kufungua biashara yangu mwenyewe.

C.M Songea

Ushuhuda wa Pili

Mshauri wangu na mwombaji mwenzangu. Amenifundisha kujua namna ya kusoma neno la Mungu na kulitafakari na kulifanyia kazi. Nimejifunza kwake namna ya kumtegemea Mungu katika kila hali ninayopitia. Maisha sasa kwangu ni mepesi zaidi ya vile nilivyokuwa nikitegemea akili zangu.

Stress zimeondoka na sasa naishi maisha ya Amani.

J. S. Mbezi Beach

Ushuhuda wa Tatu

Ukundi amenifundisha kuishi maisha ya kujiona vile neno la Mungu linavyosema. Ingawa ninatoka kwenye familia duni, lakini kwa sasa nimejifunza kuliangalia na kutamka ahadi za Mungu katika maisha yangu na hakika nimemwona Mungu akinibadilisha. Fikra zangu na Imani yangu imekua kwa kuona jinsi Mungu anavyoniona ndivyo nilivyo.

Niko huru sasa mbali na kujiona duni na niliyeshindwa kutokana na historia yangu na wazazi wangu. Sasa najiona mwenye uwezo na nguvu na ninayaweza yote katika yeye anitiae nguvu. Mimi ni mshindi katika kila eneo la maisha yangu.

R.M Tabata

Ushuhuda wa Nne

Ukundi ni radki yangu. Alikuja na mume wake Marekani kututembela na walikaa nyumbani kwetu kwa siku mbili. Ukundi alitupa neno asubuhi moja kabla ya chai na ni kama alikuwa anajua tunahitaji neno la kutu-vusha. Alisema nawaachia neno hili katika nyumba yenu 1Mambo ya Nyakati 4:10 nalo linasema "Huyo Yabesi akamlingana na Mungu wa Israel, akisema, lau kwamba ungenibarikia kweli kweli na kunizidishia hozi yangu… Naye Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba"

Tuling'ang'ana na hilo neno tukilitamka na kuliomba kwa miezi mitatu hivi. Nashukuru Mungu kitu tuli-chokuwa tunaomba tumepata na zaidi. Ashukuriwe Mungu aliye juu kwa uaminifu wake katika neno lake.

F.M USA

Ukiwa na ushuhuda wowote baada ya kusoma kitabu hiki na kukifanyia kazi, ntaomba unishirikishe kwa kupitia mawasiliano haya hapo chini. Nitafurahi kusikia kutoka kwako.

Mobile: +255 621 884 449
Email: integritythewaytosuccess@gmail.com

Facebook: ukundievans
Instagram: mafanikio workshops ongezea
Blog: www.narrowgater.blogspot.com
Website: www.vowelslimited.co.tz

Kuhusu mwandishi

Ukundi Evans Mlelwa ni mwanzilishi wa **Mafanikio Worshops,** program inayofundisha watu kuweza kupata mafanikio yao kwa kutumia mbinu zilizoko katika neno la **Mungu** (biblia) www.vowelslimited.co.tz.

Ni mwanzilishi wa **EVUK Group**, kampuni inayo-wasaidia wafanyabiashara wadogo na wakati (SME) kutengeneza mifumo katika biashara zao. www.evuk-group.co.tz.

Ukundi anafundisha watu kuishi neno la Mungu kwa kupitia rekodi zake za **Maisha Ndani Ya Kristo series 1, 2 na 3. Youtube: ukundievans**

Ameandika vitabu ambavyo ni **A believer of Jesus Christ** na **Gems of Victorious Living**.

JIPATIE CD's

Zenye mafundisho yatakayokusaidia kuongeza kasi ya kukua kiroho. Piga namba 255 621 680 439

Vitabu vingine vya mwandishi

Vinapatikana kwa softcopy.

Piga namba 255627868844331 kupata vitabu hakika yako sasa



A BELIEVER OF JESUS CHRIST

ISBN:978-9976-59-928-2

This book will show who you are in Jesus Christ, how to trust God in every situation, how to live a holy life and how to hear God in your life.

Vitabu vingine vya mwandishi

Vinapatikana kwa softcopy.

Piga namba 255 678 804930 kupatiwa kakalayokasa



GEMS OF VICTORIOUS LIVING
ISBN 978-9976-5606-0-2

This book will discuss the things that are needed to be done in your part in order for you to be in total agreement with God the Father, The son Jesus and by the help of the Holy Spirit. By doing so, we will start living a life that is Victorious, alive and well here on earth.